

**MWONGOZO**

**102/1**

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 1**

**INSHA**

**MACHI /APRILI 2015**

**Muda: Saa  $1\frac{3}{4}$**

**MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA 2015**

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

**KISWAHILI**

Karatasi ya 1

**INSHA**

Saa  $1\frac{3}{4}$

**MWONGOZO**

1. Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na rais kuzamia suala hili. Andika ripoti

### **Muundo.**

- ✓ Hii ni insha ya ripoti rasmi.

### **Kichwa**

- ✓ Anwani andikwe kwa herufi kubwa na iwe kamilifu.
- ✓ Anwani ibaini kiini cha ripoti(suala kuu linalochunguzwa)
- ✓ Bainisha kipindi cha ripoti

### **3.0 Utangulizi**

- ✓ Mteuzi
- ✓ Haja au sababu
- ✓ weka wazi muda ambao uchunguzi ulifaa kuchukuwa
- ✓ Wahusika (majina ya wanachama yaorodheshwe kuanzia kwa jina la mwenyekiti).

### **2.0 Mbinu za kukusanya data**

- ✓ Kuzuru
- ✓ Kuhoji
- ✓ Hojaji.

### **3.0 Matokeo**

- 3.1 mishahara midogo
- 3.2 mazingira magumu ya kikazi
- 3.3 ukosefu wa vifaa muhimu vyta kazi
- 3.4 mapendeleo kazini
- 3.5 uwepo wa sheria/kanuni kandamizi

3.6 Ukoefu wa kandarasi

3.7 Dhuluma za mapenzi

3.8 Ufisadi

3.9 kufutwa /kucheketwa kwa wafanyakazi

3.10 kucheleweshwa kwa marupurupu ya uzeeni

#### **4.0 MAPENDEKEZO**

4.1 Pana haja ya kubuni utaratibu wa kuimarisha mishahara ya wafanyakazi

4.2 Washika dau kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi ni wezeshi

4.3 Kuwepo kwa vifaa muhimu vya kazi

4.4 Kuwe na hali ambapo wafanyakazi wote wanachukuliwa sawa kazini

4.5 Maadili ya kikazi kuzingatiwa

4.6 Kubuniwa kwa sheria zisizovunja motisha ya wafanyakazi

4.7 Kila mfanyakazi kupewa kandarasi kama njia ya kuonyesha uthabiti wa kazi

4.8 Wafanyakazi wanaostaafu kupewa marupurupu yao kwa wakati ufaao

4.9 Waajiri kukoma kuwafuta/kuwacheketa wafanyakazi kiholela

#### **5.0 Hitimisho**

- ✓ Ripoti ihitimishwe kwa kufanya rejea ya matokeo ya utafiti
- ✓ Jopo lioneshe namna ambavyo utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa taifa kwa jumla hasa katika mchakato wa kupunguza au na kuondoa kabisa migomo ya wafanyakazi nchini.
- ✓ Tume idhihirishe wazi kuwa kubuniwa kwake kulikuja kwa wakati unaofaa
- ✓ Katibu aonyeshe ni vipi ambavyo utafiti huu utasaidia katika kuzuia migomo katika siku za halafu

**Kitambulisho** – Ripoti imeandalisha na;

- ✓ Sahihi
- ✓ Jina
- ✓ Cheo
- ✓ Tarehe .

#### **Tanbihi.**

1. Asipozingatia muundo wa ripoti aondolewe alama 4 za sura.  
Lazima awe na vipengele vinne au zaidi.
2. Hoja zisipungue tano la sivyo atakuwa amepungukiwa kimaudhui.
3. Mtahiniwa atimize urefu wa insha.(**Maneno 400**) Viwango mbalimbali vya urefu vizingatiwe katika kumkadiria mtahiniwa.
4. Jina la mwanafunzi lijitekeze kama katibu la sivyo atakuwa amepungukiwa kimtindo.
5. Atakayeandika ripoti ya kawaida na awe amezungumzia vipengele hivi atakuwa amepotoka – **Atuzwe D 03/ 20.**

6. Atakayekosa kujihusisha katika uandishi wa ripoti atakuwa amejitungia swali. **Atuzwe D – 02/20**

2. Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili

Hili ni swali la kujadili. Mtahiniwa anahitajika ashughulikie pande zote mbili za mada.

- Mtahiniwa aweza kukubaliana na mada kuwa kwa kiwango kikubwa maendeleo duni yamechangiwa na ufisadi na kuwepo kwa ufisadi au aonyeshe kuwa si kwa kiwango kikubwa vile kwani kuna sababu nyingine zinazochngia maendeleo duni nchini.
- Kwa vyovoyete vile, pande zote za mada zishughulikiwe. Haililishi kama upande mmoja utakuwa na hoja nyingi kuliko upande mwingine.

Baadhi ya hoja ni:

**Kuunga mkono**

- Kwa sababu ya hongo, kiasi fulani cha pesa za miradi hutolewa kama hongo. Hali hupunguza kiasi cha pesa za kutelezeza mradi husika.
- Kwa sababu ya ufisadi, utekelezaji wa miradi huwa wa kiwango cha chini.
- Wanaofaa kuhakikisha kuwa kuna viwango vya juu vya utekelezaji wa miradi huhongwa na hivyo kuidhinisha kazi duni.
- Kandarasi za miradi ya maendeleo hutolewa kwa wanakandarasi fisadi ambao pengine hawana ujuzi katika kufanikinisha mradi husika au ambao watatumia vifaa duni ili faida yao iwe kubwa.
- Wafadhili hukataa kuipa nchi pesa za kufadhili miradi fulani kwa hofu ya pesa hizo kutumika vibaya, hivyo basi miradi mingi haipati pesa za kutosha.
- Kuna ubadhirifu wa pesa za miradi na wanaosimamia hazina za maendeleo hivyo kuinyima miradi ya maendeleo pesa zinazohitajika.

**Kupinga**

- Hakuna pesa za kutosha nchini za kufadhili miradi mingi ya maendeleo.
- Utekelezaji mbaya wa miradi waweza kutokana na ukosefu wa vifaa bora nchini kwa hivyo vinavyotumiwa vikawa na matokeo duni.
- Kwa sababu ya siasa, miradi ya maendeleo ikatelezwa visivyo hasa katika sehemu ambayo ni ngome ya mpinzani.
- Wakati mwingine pesa za kutekeleza miradi hutumika kununulia vitu kama magari, kulipa mishahara, kulipa marupurupu nk badala ya kugharamia miradi.

**TANBIHI**

**Zingatia hoja zozote nyingine mwafaka.**

3.Baniani mbaya kiatu chake dawa.

Maana.kiatu cha baniani ni kitu au kundi la watu limechukia au kudharau

Dawa: Kitu husika huendakikawa ndicho jibu au jawabu au suluhisho kwa tatizo fulani maishaninmwa mtu au katika jamii

Mtahiniwa aandike kisa kuthibitishabmatumizi haya ya methali

Mtahiniwa nyingine zenyе maana sawa ni;

-Matango na matikiti ndio maponya nja

-Wembamba wa reli gari moshi hupita

-Nyumba nzuri si mlango fungua uingie

#### Utuza

(i) Pande zote za methali zishughulikiwe.Anayeshughulikia upande moja asipite alama C 08/20

Anayetaja tu upande wa pili bila maelezo kikamilifu achukuliwe kuwa amelenga lakini ana udhaifu wa maudhui

(ii) Anayekosa kulenga katika kisa chake amepotoka kimaudhui alama D 03/20

#### Swali la nne

Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa maneno aliyopewa

Kisa chake kifungamane na mawazo ya kauli aliyopewa

Kisa kilenga tukio lilizua taharuki mionganoni mwa wahusika

Tukio lenyewe lazima lidhiirishe maafa /maangamizi

Lazima litokee kwenye sehemu iliyozingirwa kama vile ndani ya nyumba,katika gari n.k

Mtahiniwa atumie nafsi ya tatu hali ya wingi(warejelewa)

Atumie wakati uliopita.



## MOKASA 2015

**102/2**

### MWONGOZO

#### UFAHAMU

- (a) Changamoto za Ugatuzi/Matatatizo ya ugatuzi/Ugatuzi (**alama 1x1=01**)
- (b) - Ugatuzi ni mfumo geni. (**Alama 3x1=03**)
  - Serikali kuu kutowajibika
  - Kudai kuwa mfumo huu unahitaji mda zaidi
- (c) - Mfumo wa ugatuzi nchini umehusishwa matendo ya kibepari kama vile; (**alama 3x1=03**)
  - Raia kupewa mzigo wa kulipa ushuru ili kuipa serikali mapato
  - ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi
  - viongozi kuwanyoya raia walio maskini
- (d)
  - Hali mbaya ya muundo msingi (**alama 4x1=04**)
  - Viongozi kuendeleza ufisadi
  - Ukosefu wa usawa katika ugavi wa rasilimali
  - Viongozi kupuuza mchango wa wananchi
- (e)
  - Raia kulazimishwa kulipa ili kuona maiti za jamaa zao katika fuo (**alama 2x1=02**)
  - Raia kurundikiziwa mzigo wa kulipa ushuru mkubwa
  - Ushuru unaolipwa na wananchi hauwasaidii wananchi ila huishia mifukoni mwa viongozi
- (f) (i) Ugavi wa mamlaka na rasilimali kutoka serikali kuu hadi mashinani (**alama 2x1=02**)  
(ii)mfumo wa kiuchumi wa watu wachache kumiliki rasilimali kwa kuwapora wengine

*Ondoa nusu alama kwa kila kosa la sarufi hadi makosa sita.*

*Ondoa nusu alama kwa kila kosa la tahajia hadi makosa sita.*

### UFUPISHO

**(a)**

- ✓ Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu
- ✓ Viwanda vikubwa hupata ugumu kufanya biashara katika masoko finyu
- ✓ Viwanda vidogo vinaweza kuwaajiri wafanyakazi wengi

- ✓ Kuanzisha viwanda hakuhitaji mtaji mkubwa
- ✓ Ni rahisi kujaribisha bidhaa katika kiwango kidogo cha kiwanda kidogo
- ✓ Viwanda vidogo huchochea usambazaji wa viwanda mashambani
- ✓ Hii husababisha ajira kusambazwa nchini
- ✓ Usambazaji huleta mweneo wa mapato kote nchini
- ✓ Huu ni msingi wa maendeleo
- ✓ Viwanda vidogo ni msingi wa kujitegemea kiuchumi

(b)

- ✓ Tatizo la kwanza ni mtaji.
- ✓ Ukosefu wa mikopo ya muda mrefu
- ✓ Mikopo ya muda mfupi inatozwa riba kubwa
- ✓ Lipo tatizo kubwa la kawi
- ✓ Gharama ya umeme huenda iwe ya juu
- ✓ Ukosefu wa maarifa ya kibiashara na ujasiriamali

|   |        |                                 |
|---|--------|---------------------------------|
| M | a – 8  | $s - 6 \times \frac{1}{2} = 03$ |
|   | b – 5  | $h - 6 \times \frac{1}{2} = 03$ |
|   | ut – 2 | $z - \text{maneno } 10 \ 1z$    |

### MATUMIZI YA LUGHA

- a) Majuso ya majijana yale yalichujuka yalipoanguka ( $4 \times \frac{1}{2}$ )
- b) Akisoma kwa bidii, atapita mtihani  **$2 \times 1 = 02$**   
Akirauka mapema, atapata basi  
**(lazima pawepo na vitenzi viwili)**
- c) Abudu-Abudishiana  **$1 \times 2 = 02$**   
Mf Wapenzi wale waliabudishiana baada ya kufunga nikahi.
- d) "Aisee! Yale mawimbi ya Tsunami (yaliyotokea Bahari Hindi) yaliangamiza biashara nyingi sana."  
Alisema Bomet. **(Vitahiniwa  $8 \times \frac{1}{2} = 04$ )**
- e) S\_\_S1+U+S2  
S1\_\_KN+KT  
KN\_\_N  
N\_\_Rais  
KT\_\_T  
T\_\_Alihutubu  
U\_\_lakini  
S2\_\_KN+KT

KN\_\_O

KT\_\_T

T\_\_Walimpuuza. **8x ½**

- f) Kishazi huru hutoa maana iliyokamilika. Ni sentensi sahihi (alama 3)  
Kishazi tegemezinhuota maana isiyokamilika na hivyo hutegemea kingine kukamilika kimaana  
Mf. Ingawa alifunza vizuri, walifeli mtihani.

**k.t                            k.h**

- g) Ni sentensi agizi (ya masharti) **2x1=02**

Au

Ni sentensi ya kuamuru (ya masharti)

- h) K.m Kaondokeni (**kadiria**) **1x1=01**

- i) (i) chagizo-neno/maneno ambayo huchukua nafasi ya kielezi katika sentensi. **(2x1=02)**  
Kikiondolewa hakithiri maana ya sentensi

(ii) chagizo- Haraka **(1x1=01)**

- j) Mzee Kambumbu alisema kuwa kile kijicho cha paka cheupe, siku hiyo kingekuwa marufuku kwake. **(6x ½ =03)**

- k) Zawadi(N)- zawidi(T)

k.m Alizawidiwa kwa kupasi mtihani **(1x2=02)**

- l) Jino Ngeli ya LI-YA **(4x ½ )**

i. Jitu-ukubwa/uduni wa kitu

ii. Kujilia-kirejeshi/kujirejelea

iii. Mkimbiaji-mazoea/uzoefu

- m) Ilimradi-ili,iwapo,kwa masharti kwamba,mradi. **(Alama 1x2=02)**

Mf. Nitaruka maji ilimradi nipewe zawadi

- n) Kihisishi cha bezo k.m mmm! Po! Nyoo! Mnh! Ngoo! Mawe! Ebo! Wapi! Zii! Aka! **1x1=01**

- o) Wa- nafsi **(alama 4x ½ =02)**

li-wakati uliopita

an-kauli ya kutendana

a-tamati

- p) Kiimbo-ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji **(alama 1x1=01)**

Ni kiwango cha utoaji wa sauti kutegemea ujuu na uchini wake unaowezesha kupata tofauti za hisia za msemaji

- q) (i) Vokali- ni sauti zinazotamkwa hewa inapotolewa bila kikwazo/kuzuiliwa **(alama 1x1=01)**

(ii) /i/ ni sauti ya mbele ya kinywa **(alama 2x 1 =02)**

Ni sauti ya juu ya kinywa

Midomo hutandazika inapotamkwa

r) Kugawika kwa njia (**Alama 2x1=02**)

Ingia katika chombo cha kusafiria

Paji la uso

Pembe kubwa inayopigwa nchani

Manati/chombo cha kurushia mawe

### **ISIMUJAMII**

a)

- ✓ **Kiswahili ni lugha ya Kibantu** - Lugha ya Kiswahili ina maneno mengi ya Kibantu hivyo basi chimbuko lake ni Kibantu.
- ✓ **Kiswahili imetokana na lugha ya Kiarabu** - Lugha hii ina maneno kadha ya Kiarabu. Hii yaonyesha kuwa ni lugha ya Kiarabu.
- ✓ Kiswahili ilitokana na **mchanganyiko wa lugha ya Kibantu na Kiarabu** - Maneno mengi ya Kiswahili yana asili ya aidha Kibantu ama Kiarabu. Hii yaonyesha kuwa lugha hii ni uzawa wa lugha hizi mbili. (**Hoja 3 x 2 = 6**)

b)

- i. **Uwili lugha-** uwezo wa mtu kuzungumza lugha mbili
- ii. **Lingua Franka-** lugha inayounana na mazingirganisha watu wanaozungunza lugha tofauti
- iii. **Misimu-** semi za mda zinazotumika na kikundi fulani cha watu na hutoweka kwa baada ya mda.
- iv. **Sajili-** matumizi ya lugha kulingana na mazingira

**4x1=04**

### **Jinsi ya kusahihisha matumizi ya Lugha**

- Ondoa nusu ( $\frac{1}{2}$ ) kwa kila kosa la sarufi (s) litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu alama ( $\frac{1}{2}$ ) kwa kila kosa la tahajia (h) litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita katika swali lote yaani:

**( $6 \times \frac{1}{2} = 03$  )**

### **Jinsi ya kusahihisha Isimu Jamii**

- Ondoa nusu ( $\frac{1}{2}$ ) alama kwa kila kosa la sarufi (s) litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata (si alizotengewa) katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu ( $\frac{1}{2}$ ) alama kwa kila kosa la hijai (h) litokeapo kwa mara ya kwanza hadi makosa sita yaani

**( $6 \times \frac{1}{2} = 03$  )**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA  
KISWAHILI KARATASI YA 3  
FASIHI  
MOKASA 2015**

**1. Misimu**

Misimu ni semi za muda ambazo hubuniwa katika mazingira maalum katika kipindi maalumu cha wakati. Misimu pia huitwa simo. Misimu inaweza kupata mashiko katika jamii na kukubaliwa kama msamiati au semi rasmi za lugha. (alama 2)

**Sifa za misimu**

- (a) Misimu ni semi au msamiati ambaeo huzuka na kutoweka baada ya muda Fulani.
- (b) Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao katika kipindi Fulani cha wakati na mahali Fulani.
- (c) Hutumiwa na kundi Fulani la watu kufanikisha mawasiliano. Kwa mfano, kuna misimu ya vijana, ya wafanyakazi katika vyombo vya usafiri na hata ya watoto.
- (d) Ingawa misimu huzuka na kutoweka baada ya muda, baadhi ya misimu hudumu na kukubalika kama semi au msamiati sanifu wa lugha husika. Kwa mfano, neon chai (kama maana ya hongo) lilianza kama msimu, kasha likashika na kukubalika kama mseimi sanifu.
- (e) Misimu hupata maana yake kutoka kwa watumiaji pamoja na kmuktadha wa mahali au wakati. Kwa mfano, neon sare ni msimu uliopata maana katika sera ya usafiri wa matatu likamaanisha kubebwa bila malipo. Aidha, pauni ya Uingereza ilipokuwa thamani ya shilingi ishirini za Kenya, noti ya shilingi ishirini ilirejelewa kama pauni. Baada ya mabadiliko ya wakati na kiuchumi, ilikuja kurejelewa kama mbaeo. Huenda neon hili litabadi lika tena au liusalie hivyo.
- (f) Misimu si semi sanifu, hivyo haipaswi kutumiwa katika miktadha rasmi.
- (g) Misimu huundwa kwa mbinu mbalimbali kama vile kutohoa maneno au kugeiuza mpangilio wake, kwa mfano risto (hadithi) kutoka neon ‘story’ la Kiingereza.

(5X2=10)

**Dhima ya misimu**

Misimu hutumiwa kutekelea majukumu mbalimbali katika jamii, kama ifuatavyo:

- (a) Ni kitambulisho cha kundi Fulani la watu. Misimu ya mabaharia, kwa mfano, huwatambulisha na kuwatofautisha mabaharia na vikundi vingine vya wafanyakazi katika vyombo vya baharini kama vile makuli.
- (b) Misimu huhifadhi siri za wanaoitumia. Watu hutumia misimu ili kulinda siri zao zisijulikane.
- (c) Hutumiwa kuibua hisia mbalimbali mionganoni mwa wazungumzaji. Kwa mfano, waasisi wa wa misimu chunga na ndizi nchini Kenya wakati wa kura ya maoni kuhusu katiba mpya mwaka 2005 waliitumia misimu hii kunadia wito wao wa kupinga au kuunga mkono katiba hiyo.
- (d) Hukuza ushirikiano, uzalendo na uaminifu mionganoni mwa wanaoitumia. Lugha ni nyenzo kuu ya kuwaunganisha watu, hivyo wanajamii wanapotumia misimu sawa, hujiona kuwa na mionjo, hali na maazimio sawa.
- (e) Huongeza haiba au ladha katika lugha, hivyo kuondoa ukinaifu unaotokana na kutumia msamiati uliozoleka miaka nenda miaka rudi.
- (f) Hutumia kupunguza makali katika lugha au kutasfidi lugha. Badala ya kutumia neon la aibu au msamiati unaoibua masikitiko, watu hubuni misimu kueleza jambo kwa njia nyepesi isiyoumiza.
- (g) Hukuza lugha zaidi. Wakati mwengine misimu hukubalika kama msamiati rasmi, misemo, methali au nahau katika lugha Fulani. Kwa mfano, maneno matatu na daladala ni misimu iliyobuka kurejelea magari ya uchukuzi wa umma nchini Kenya na Tanzania mtawalia. Kwa sasa, maneno haya yanakubalika kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiswahili.

- (h) Huhifadhi utamaduni na historia ya jamii. Kwa vile misimu tofauti hutumiwa katika vipindi mbalimbali vya wakati, kuwapo kwake huakisi maendeleo, ukuaji, historian a mabadiliko katika jamii husika.
- (i) Ni kielelezo cha mpangilio (mfumo) wa jamii Fulani, kijamii na kiuchumi. Kwa vile misimu hutambulisha matabaka katika jamii, tunaweza kutambua ni matabaka gani yanayounda jamii hiyo.
- (j) Hutumiwa kuondoa urasmi katika mazungumzo. Vijana, kwa mfano, wanapotumia misimu badala ya semi sanifu, huondoa urasmi na kudumisha uhusiano wa kirafiki.
- (k) Hukuza uwezo wa kufikiri na kutathmini au kudadisi. Ili kuelewa misimu Fulani, ni lazima ufikirie na kutathmini chanzo cha msamiati huo. Mathalani Mukoloni (mama) ni mfano wa msimu wa nyumbani. Ili kuelewa, inabidi ufikirie zaidi na kupima ni nani aliye na tabia za kudhibiti watoto zaidi kati ya mama na baba. (4X2=8)

## 2. **SEHEMU A: TAMTHILIA MSTAHIKI MEYA**

- (a) Maneno haya yanasemwaa na Bili  
Anamwambiya mstahiki Meya.  
Wamo afisini mwa Meya.

Ni baada ya Meya kumshukuru Bili kwa Ushauri aliompa uliomwezesha kuwa Meya na mara hii anamtaka Bili kumshauri kumhusu mwanakandarasi ambaye ameenda mahakamani kumshtaki kwa kuvunja mkataba kinyume na sheria.(4X1=4)

- (b) Takrirri/Urudiaji-Tumbo (alama 2)

- (c) Mzungumzaji – Bili
- i. Mshauri mbaya
  - ii. Mwenye majisifu
  - iii. Mwenye ubinafsi
  - iv. Mpenda makuu
  - v. Ana tama
  - vi. Msaliti
  - vii. Fisadi
  - viii. Laghai
  - ix. Mnafiki
  - x. Mpenda anasa
  - xi. Barakala

(zozote nneX2=8)

Umuhimu

- i. Kielelezo cha ufisadi
- ii. Anaonyesha unafiki
- iii. Athari za ushauri mbaya

(2x1=2) (Jumla 10)

### d. Ufisadi alama 1

- i. Wakati meya. Bili na Diwani 1 na Diwani 11 wanakubaliana kuuza fimbo ya Meya ili kujipatia pesa (alama 1)
- ii. Meya kutumia cheo chake kujinyakulia mashamba na kasha kumgawia Bili vipande vine vya ardhi. (alama 1)

Maneno ya Balozi (mfawidhi) akitoa hotuba uwanjani katika siku ya kuadhimisha siku ya Wazalendo. Alikuwa akirejelea Mtukufu Mtemi Nasaba Bora. Awali alikuwa ametanguliza kuhusu umuhimu wa kuwakumbuka watu ambao walipigania uhuru ,paka nchi ikawa huru. Aliendelea kumpa sifa zaidi Mtemi Nasaba Bora kasha kamkaribisha Mtemi kuhutubia umati wa watu. (4X1 = 4)

b. Ni kinaya kwa sababu

- Mtemi Nasaba Bora hakuywa na utu na fadhili. Alikuwa katili sana.
- Hawakuwakumbuka waliopigania uhuru, baadaye familia zao ziliteswa na kunyang'anywa mashamba yao na hata kuuawa.
- Mtemi Nasaba Bora aliwaweka wananchi katika ukoloni wa aina nyingine.
- Ukoloni mamboleo. Hakuwakomboa. (4X1=4)

c.

- **Askari.** Askari walitumiwa kuwadhulumu watu, kuwapiga na kuwalazimisha kuhudhuria mikuutano ya Mtemi. Wanatumiwa kuwashika wale waliopinga Mtemi. K.m Matuko Weye. Ilibidi watu kuongea kwa sauti za chini wakati wa sherehe kwa sababu ya askari. Iliwabidi watu kuhudhuria mkutano. Askari walifika kidandani kujua ni kwa nini Imani hakuhudhuria sherehe. Askari wa Mtemi walijihimu mapema kwenda kuwatia mbaroni Amani na Imani kwa tuhuma za uuaji wa kitoto kichanga, Uhuru. Askari walitumwa kwa mamake Imani ili kumtoa katika shamba lake kule Baraka. Walitumiwa kuwafanya kazi Imani na Amani gerezani.
- **Jela.** Amani na Imani walipigwa na kutiwa ndabi kwa tuhuma za kusababisha kifo cha motto Uhuru. Matuko Weye alifungwa kwa sababu wakati wa sherehe alikichukua kipaaza sauti na kusema kuwa walikuwa wamedhulumiwa na viongozi na ilikuwa wakati wa Wanatomoko kujikomboa. Mtemi Nasaba Bora alimfungisha Yusufu ili asitoe siri kuwa mtemi alinyakua ardhi ya Chichiri Hamadi.
- **Propaganda** – Kufumia ndugu yake mhariri kumlimbikizia sifa.
- **Vibarakala.** Maozi alikuwa kibarala wa Mtemi. Alimpa Mtemi sifa nyingi za uongo hasa wakati alipokuwa mfawidhi katika sherehe za sikukuu ya wazalendo. Maozi pia alikuwa na mazoea ya kusema mambo aliyotakiwa kuyasema. Hii ndiyo sababu iliyomfanya kuhifadhi kiti cha ufwidhi kwa miaka mingi.
- **Majaji.** Ili kumfungisha Yusufu kwa sababu ya kumuua babake ilimbidi Mtemi Nasaba Bora kuwalipa makarani wa mahakama na majaji.
- **Majangili.** Mtemi akiwa katika wizara ya ardhi na makao aligundua Chichiri akiwa London alikuwa amenunua shamba la mzungu. Aliwalipa majambazi kummaliza pindi alipowasili nchini./Walimvua.
- **Vitisho.** Wananchi walitishwa na kuwaogopa viongozi wao. Walishuhudia wenzao wakudhulumiwa kimya kimya.
- **Asasi za serikali.** Mtemi alijigawia mashamba akitumia wizara ya ardhi. Pesa za mahawinde na zahanati ziliibiwa. Serikali huru ilipoanzishwa sera za kuwapa Waafrika makao katika sehemu zilizotengewa wazungu, Mtemi Nasaba Bora alitengeneza faili ili zimfae yeye.
- **Hongo-** Mahakama, polisi.

5. (d)

**Sadfa**

Hii ni mbinu ya matukio mawili au zaidi kutokea wakati mmoja bila kupangwa. Sadfa huathiri mkondo wa hadithi kwani huathiri matukio ya baadaye. Tazama mifano ifiuatayo:

- i. Imani anakutana kisadfa na Amani pale Ziwa Mawewa wakati Imani ameamua kujiua. Imani anaghairi kujiua na kuandamana na Amani huko Sokomoko.
- ii. Imani na Amani wanapokutana, wote wameharibikiwa kwao. Amani amekuja Ziwa Mawewa akutosa mswada wake uliokataliwa na wachapishajo, naye Imani amukuja kujitosa ziwani kwa

sababu ya kufiwa na mama na kuchomewa nyumba. Amani anaweza kumwambia Imani anakwenda Sokomoko kutafuta ajira ya shamba nae Imani anasema wataandamana. Huu unakuwa mwanzo wa uhusiano wao.

- iii. Inasadifu kwamba Amani na Imani wanakutana na DJ pale Mto Kiberenge. DJ anaweza kuwaelekeza kwa Nasava Bora na Majisifu.
- iv. Inasadifu kwamba wakati Bi Zuhura anapomwita Amani chumbani mwake ndipo Nasaba Bora anaporudi nyumbani na kuwafumania. Ndoa ya Nasaba Bora inasambaratishwa na tendo hili. Ukatili wa Nasaba Bora unabainishwa na kipigo anachompa Amani.
- v. DJ anapita karibu na kibanda cha Amani wakati Amani anapowazia atakalofanya kuhusu kile kitoto. Amani namtuma DJ kumwomba Imani kuja kumsaidia kwa malezi ya hiki kitoto.
- vi. Inasadifu kwamba kulipa kisasi kwa Nasava Bora. Amani anafanikiwa kumkataza Oscar asilipize kisasi. Tendo hili linambadilisha Nasaba Bora. Anaomba msamaha na kumpa Amani hatimiliki za mashamba aliyoiba.

## 6. USHAIRI

- a) Ujumbe ni kuwa asiyekuwa na mali hathamanini. (alamu 1)
- b) Kusisitiza kwa ujumbe
  - i. Kueleza vile sultan, shere, walimu walivyopungua thamani.
  - ii. Mkono mtupu haulambwi.
  - iii. Azizi kuwa kama wapuuzi.
  - iv. Makubeli kuwa kama nyani.(1X3=3)
- c) **Muundo wa shairi.**
  - i. Lina beti nne.
  - ii. Lina mishororo sita.
  - iii. Kina kimoja katika mshororo.
  - iv. Vina vinalingana kila baada ya unaofuata ubeti.
    - 1. Ki,ni,ni,ki,ni
    - 2. Zi,ni,zi,ni,zi,ni
    - 3. Li,ni,li,ni,li,ni
    - 4. Mu,ni,mu,ni,mu,ni(zozote 4X1= alamu 4)  
(1X4 =4)
  - v. Shairi lina kiishio
- d) Wahenga walisema kuwa mkono mtupu haulambwi. Anasema kuwa duniani ukiwa huna kitu basi huthaminiwi. (alamu 3)
- e) **Idhini ya kishairi.**  
Inkisari – ta'bani badala ya taabani kuboronga sarufi – Duniani husifiki. (2x2= alamu 4)
- f) **Mbinu za lugha**
  - I. Methali -Mkono mtupu haulambwi.
  - II. Tashibibihi - Wamekuwa kama nyani
  - III. Bhalagha -Yalisemwa hukumbuki?
  - IV. Misemo -Bila kitu kiganjani.(Zozote 2X1 = alamu 2)
- g) **Maana ya maneno**
  - I. Kukirimu - Kufanyia wema, fadhili.
  - II. Makubeli - Watukufu, wakubwa, wenye vyeo.
  - III. Mahashumu -Waheshimiwa, watukufu, makubali.(1X3 = 3)

## 6 . USHAIRI

(a)

- I. Anasa
- II. Hadaa na dunia
- III. Kuyaacha mabaya
- IV. Kunyetea dunia
- V. Pupa

(zozote 4X1 = 4)

(b)

- i. Mashujaa- waliotukuka kwa nguvu mwisho wakafedheheka.
- ii. Mahuluki – Waliokuwa na mali lakini wakayaacha.
- iii. Matajiri – waliokuwa na ngwenje mwishowe wakafa na yao kupotea.
- iv. Waliosifika wakiishi ghorofani, mwishowe kufukiwa na udongo.

(zozote 4X 1 = 4)

(c) (i) Inkisari (kufupisha maneno)

|           |   |              |
|-----------|---|--------------|
| Ndu yangu | - | ndugu yangu  |
| Yataka    | - | inataka      |
| Walokuwa  | - | waliokuwa    |
| Wanenalo  | - | wanalolinena |
| Zilosalia | - | zilizosalia  |
| Kawafukia | - | ukawafukia   |
| Turudipo  | - | tunaporudi   |
| Walizo    | - | walizokuwa   |

(ii) Tabdila (kubadili sauti)

|                  |   |             |
|------------------|---|-------------|
| Mf. Kutwepushiya | - | kutuepushia |
| Kujifichiya      | - | Kujifichia. |

(iii) Mazida

|                |                        |
|----------------|------------------------|
| Mf. Siwelewele | – Usiwele.             |
| Hoja mbili     | zitolewe mifano miwili |

2X2 =4

(d)

Kuna watu ambaa waliishi ghorofani. (Yaani nyumba nzuri zilizokuwa na mapambo na mazulia) lakini sasa wameyaachia marafiki na jamii mali yao yote. Sasa matajiri wale wameshafariki wamo makaburini.

Anamalizia kwa kusema kwamba dunia ni mbovu, unaweza kusumbuka ndugu yangu usiilewe.

(alamu 4)

(e) (i) Nazaa- aibu, fedheha

(ii) Kam Kam – kwa mfano, mfano wa  
(iii) Tatughofiria – atakusamehe.  
(iv) Madhaifu – wakawa bure.

(alamu 4)

## 8. SHAKA YA MAMBO

Shaka ni wasiwasi/ wahaka kuhusu jambo.

Hadithi inaeleza hali ya mashaka katika maisha yanayomzunguka Esther.

Mifano

- I. Pana shaka ya mambo kuhusu yeye kufikia lengo lake la kusomea ukatibu muhtasi kwa ukosefu wa fedha.
- II. Pana shaka kuhusu uhusiano wake Kamata ambaye Anaonekana kutojali.

- III. Pana shaka iwapon Kamata na Grace wana uhusiano au la.
- IV. Shaka pale ambapo Grace anaonekana kuwa na miadi ya Kutoka wakatembee na Kamata.
- V. Shaka iwapo Kamata angemkaribisha kiti alivyofanya mvulana mel garini.
- VI. Esther anaona skaka katika kufanya kazi ambayo siyo aliyoijia mjini.
- VII. Shaka kwamba hana uhuru wa kutembea Nairobi atakavyo na Saa atakazo.
- VIII. Esther ana shaka kuhusu usalama wa vilabu vya Nairobi japo anatamani kwenda diskoo.
- IX. Ana shaka na hali ya kuamka alfajiri kwenda siku sita kwa wiki.
- X. Shaka na hali ya kuamka kuahidiwa angebadilishiwa zamu kazini – amefanya mfululizo kwa miezi mitatu.
- XI. Alikuwa na shaka kumwoa Kamata akimkonyeza Grace.
- XII. Esther alishuku kusisitiza kwa Kamata kuwa ampe pesa kumpelekea mteja Yule hata akasita kumpa.
- XIII. Esther alikuwa na shaka kwa namna Kamata angemjua mzungu Yule bila Esther kumwelezea sifa zake.
- XIV. Esther alikuwa na shaka alipokosa kumwona Kamata kazini siku hiyo waliokuwa na miadi na